KATIKA MAHKAMA KUU YA ZANZIBAR

IMESIKILIZWA TUNGUU

RUFAA YA MADAI NAM. 16 YA 2022

(KUTOKA RUFAA YA MADAI NAM. 19 YA 2021 (KADHI WA RUFAA) NA KESI YA MADAI NAM. 618 YA 2020 (KADHI WA WILAYA MWANAKWEREKWE))

KADIR YUSSUF MUHIDIN … … MKATA RUFAA

(akiwakilishwa na wakala wake Wanu Ali Mohamed)

DHIDI YA

ASRAA SAID KHALID … … MPINGA RUFAA

HUKUMU

TAREHE YA HUKUMU: 19.1.2023

MBELE YA: MHESH. ISSA, A. A., J

SHEIKH SAMEER ZULFIKAR

SHEIKH SALEH HAKIM

SHEIKH JUMA FAKIH

SHEIKH KANI MKANGA

Hukumu hii inahusiana na rufaa iliyowasilishwa Mahakamani na kupewa namba 16 ya mwaka 2022. Rufaa hii iliwasilishwa na Kadir Yussuf Muhidin dhidi ya Asraa Said Khalid. Rufaa hii inapinga uamuzi uliotolewa na Kadhi wa Rufaa Sk. Hassan Othman Ngwali.

Kwa ufupi rufaa hii inatokana na Kesi ya Madai Nam. 618 ya 2020 iliyoanzia katika Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe ambayo ilisikilizwa na Sk. Abdulrahman Omar Bakar. Mdai katika kesi hiyo ni Asraa Said Khalid (Mpinga rufaa) ambae alifungua kesi dhidi ya Kadir Yussuf Muhidin (Mkata rufaa) na madai yake katika kesi hiyo kwa mujibu wa hati ya madai ni kwamba wadaawa walikuwa ni

wanandoa ambao walifunga ndoa yao tarehe 14.8.2020 lakini ndoa hiyo haikuwa na masikilizano na Mkata rufaa alimwacha Mpinga rufaa talaka tatu tarehe 13.9.2020. Mpinga rufaa alifungua kesi katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya akidai vitu viwili ambavyo ni karatasi rasmi ya talaka pamoja na vyombo ambavyo vilitolewa kama mahari. Mpinga rufaa alipelekewa talaka nyumbani kwao na hivyo vyombo ambavyo vilikuwa ni mahari aliviwacha alipokuwa akiishi. Vyombo hivyo ni kitanda cha futi 6 kwa 6 na godoro lake, kabati la milango mitatu na meza ya kujipambia (dressing table).

Mkata Rufaa katika hati ya majibu ya madai alikubali kumwacha Mpinga rufaa talaka tatu na hakuwa na pingamizi na Mkata rufaa kupewa talaka rasmi lakini alitaka iwe kwa gharama zake. Kwenye upande wa dai la kurejesha vyombo ambavyo ni mahari hili alilipinga na kudai kwamba Mpinga rufaa ametaka mwenyewe kuachwa, na hata wazee wa Mpinga rufaa walipokuja kuchukua vyombo vya matumizi vya Mpinga rufaa vyombo vya mahari waliviwacha.

Kadhi wa Wilaya, Sk. Abdulrahman Omar Bakar baada ya kusikiliza kesi hiyo alitoa hukumu yake tarehe 12. 4. 2021 kama ifuatavyo:

> *“Hivyo basi Mahkama inamuamuru mdai akavichukue vyombo vyake vya mahari kwa mdaiwa ndani ya siku 45 kwa gharama zake. Baada ya kupita siku hizo 45 alizopewa na Mahkama bila ya kwenda kuvichukuwa bila ya sababu yoyote atakayoileta Mahkamani na kukubaliwa basi itahesabika kuwa amevisamehe vitu hivyo. Lakini Mahkama inamuamuru mdaiwa amkabidhi mdai vitu hivyo vyote bila ya kikwazo chochote tena vikiwa katika hali yake ile ile aliyoiacha mdai na kama anashindwa kuvihifadhi basi anaweza kuviwasilisha Mahkamani siku yoyote ya kazi na gharama za uletaji zitalipwa na mdai.”*

Mkata Rufaa hakuridhika na hukumu hiyo na hivyo kukata rufaa katika Mahakama ya Kadhi wa Rufaa, Sk. Hassan Othman Ngwali. Kadhi wa Rufaa baada ya kusikiliza rufaa hiyo alitoa hukumu yake tarehe 1.12.2021 ambapo aliunga mkono hukumu na amri zilizotolewa na Kadhi wa Wilaya. Kadhi wa Rufaa alifikia maamuzi hayo baada ya kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Mkata rufaa amekiri kuacha talaka tatu mwenyewe tokea mwanzo wa kesi ya msingi hata hapa kwenye rufaa.
b) Katika karatasi ya talaka aliyoiandika akiwa peke yake hakuna sharti la kuacha mahari.
c) Talaka ameiandika Mkata rufaa wakati wa usiku akiwa peke yake bila ya Mpinga rufaa kuwepo au mtu mwengine yoyote.
d) Talaka imepelekwa na Mkata rufaa mwenyewe usiku huo huo kwa wazazi wa Mpinga rufaa.
e) Wanandoa hawa walikuwa na mvutano na mgogoro siku hiyo ilipotoka talaka.
f) Mpinga rufaa aliondoka kutoka nyumbani kwa Mkara rufaa kwa madai kwamba siku hiyo kulikuwa na mgogoro kati yao.

Mkata Rufaa hakuridhika na hukumu hiyo na kukata rufaa katika Mahakama hii. Amewasilisha hati yake ya rufaa ikiwa na sababu tatu za rufaa kama ifuatavyo:

1. Kwamba Mhe. Naibu Kadhi Mkuu amekosea kisheria katika hukumu yake kwa kutoa hukumu ya kukubaliana na amri ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

2. Kwamba Mhe. Naibu Kadhi Mkuu huyo msomi wa Mahakama ya Kadhi Mkuu ameshindwa kisheria kutambua kuwa kulikuwa na masharti kati ya Muomba rufaa na Mpinga rufaa; masharti ambayo Mpinga rufaa ameyavunja.

3. Kwamba Mhe. Naibu Kadhi Mkuu hakupaswa kisheria kuutilia nguvu upande wa Mpinga rufaa pekee kwa sababu tu upande huo umekataa kuwekeana sharti na kuupa nguvu upande huo bila ya kuangalia haki ya Muomba rufaa kisheria.

Mahakama hii iliwasikiliza wadaawa kuhusiana na rufaa hii. Kwa upande wa Mkata rufaa akiwakilishwa na wakala wake alieleza kwamba wamekata rufaa kwa sababu kesi ilisikilizwa upande wa Mpinga rufaa tu, upande wao haukusikilizwa. Waliambiwa warudi nyumbani na wasubiri lakini hawakuitwa tena. Baadae walipata hukumu kwamba warejeshe vitu wakati wao hawakusikilizwa. Vile vile alisema hata Kadhi wa rufaa nae alikubaliana na Kadhi wa Wilaya. Sasa hivi wamekuja hapa ili haki itendeke na hata wakiambiwa walipe basi waamriwe walipe kwa awamu kwani wao ni maskini.

Mpinga rufaa kwa upande wake alipinga suala hilo na alisema kwamba kesi haikusikilizwa upande mmoja. Kesi ilipopangwa wote walienda lakini tarehe nyengine ilipopangwa Mkata rufaa hakufika Mahkamani. Aliendelea kueleza kwamba yeye alitoa ushahidi wake lakini Mkata rufaa alipopangiwa kutoa ushahidi hakuja ndipo Kadhi alipopanga kesi bila ya Mkata rufaa kuwepo. Vile vile alieleza kwamba yeye hakuwahi kudai talaka bali baada ya mazozano alikwenda kwao na aliletewa talaka nyumbani kwao.

Wakala wa Mkata rufaa akijibu hayo alikubali kwamba ni kweli walikwenda kwenye kesi pamoja lakini jalada lilipohamishwa wao hawakupewa tarehe. Waliambiwa wataitwa lakini hawakuitwa. Walikaa miezi mitatu na baadae waliitwa Mahkamani na Mkata rufaa akatiwa pingu. Hivyo, kesi haikusikilizwa. Kuhusu suala la mahari wakala alieleza kwamba Mpinga rufaa aliachwa kwa masharti arejeshe mahari na akakubali kufanya hivyo. Vitu vya mahari vipo kwake yeye.

Baada ya Mahakama kuisikiliza rufaa hii na kupitia mwenendo wa kesi wa Mahkama ya Wilaya na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa ni wazi kwamba Mkata rufaa alimwacha Mpinga rufaa kwa talaka tatu. Suala lililopo jee kulikuwa na sharti lolote la kutoa talaka hiyo kama ilivyodaiwa na Mkata rufaa.

Kabla ya kulizungumza suala hilo kumezuka malalamiko kwamba kesi katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya ilisikilizwa upande mmoja na baadae Wakata rufaa kupewa amri ya kutekeleza hukumu iliyotolewa. Mahkama ilipitia mwenendo wa Kadhi wa Wilaya na kuona kwamba siku ya tarehe 7.1.2021 kesi hiyo iliitwa kwa kusikilizwa na Mkata rufaa na Mpinga rufaa wote walikuwepo. Mpinga rufaa alianza kwa kutoa ushahidi wake kwa kiapo, na baadae shahidi wa Mpinga rufaa, Salum M. Ali nae alitoa ushahidi wake kwa kiapo na kuulizwa masuali na Mkata rufaa. Kesi ilipangwa kuendelea kusikilizwa upande wa Mpinga rufaa tarehe 19.1. 2021 na siku hiyo Mpinga rufaa alitoa ushahidi uliomo ndani ya simu na alifunga kesi yake.

Kesi ilipangwa kusikilizwa upande wa Mkata rufaa tarehe 9.2.2021 na Mkata rufaa alitoa ushahidi wake kwa kiapo na baadae aliomba kuendelea kutoa ushahidi kikao kitakachofuata. Kesi ilipangwa kuendelea kusikilizwa tarehe 22.2.2021 lakini Mkata rufaa hakufika Mahkamani. Kesi iliakhirishwa hadi tarehe 16.3.2021 ambapo Mkata rufaa hakufika tena Mahkamani. Kesi iliakhirishwa hadi tarehe 9.4.2021 ambapo

Mkata Rufaa pia hakufika Mahakamani, na hapo Kadhi wa Wilaya ndipo alipolipanga shauri hilo kwa hukumu.

Hivyo, dai la kwamba kesi ilisikilizwa upande mmoja si la kweli; vile vile kwamba kesi ilihamishwa bila ya Mkata rufaa kujuilishwa pia si la kweli. Kesi yote ilisikilizwa na Kadhi mmoja tu ambaye ni Sk Abdulrahman na haikuwahi kuhamishwa katika Mahkama nyengine. Vile vile pande zote mbili zilipewa fursa ya kusikilizwa lakini Mkata rufaa alishindwa kuleta mashahidi wake hata baada ya Mahkama kuakhirisha kesi mara tatu. Hivyo, dai hilo halikuwa na msingi wowote.

Hata hivyo, kwa vile Mkata rufaa katika sababu zake tatu za rufaa alidai kwamba alitoa talaka kwa Mpinga rufaa ikiwa na masharti ya kuviwacha vyombo alivyopewa kuwa ni mahari. Kwa vile karatasi ya talaka haikuwa na sharti la aina yoyote Mahkama ilimruhusu Mkata rufaa kuita mashahidi wake ambao walishuhudia akitoa talaka pamoja na kuifunganisha talaka hiyo na sharti la kuviwacha vyombo vya mahari.

Mkata rufaa alimwita baba yake, Yussuf Muhidin Haji ambaye alitoa ushahidi wake na kusema kwamba Mpinga rufaa talaka kaitaka mwenyewe na kaondoka saa 5 za usiku na kwenda kwao. Yeye alimzuia lakini alikataa na kuondoka. Aliendelea kueleza kwamba yeye hana uhakika kuhusu sharti lililotolewa na Mkata rufaa. Mkata rufaa alimwacha Mpinga rufaa kwa maandishi lakini hakuyaona wala kuyasikia.

Shahidi wa pili alikuwa ni ndugu wa Mkata rufaa, Ame Yussuf Muhidin ambaye alieleza kwamba Mkata rufaa alipomwacha Mpinga rufaa yeye alikuepo nyumbani lakini hakuona talaka ikiandikwa na hukusikia sharti lolote. Mpinga rufaa alipoondoka alisema kwamba anaacha vitu vyake lakini baadae alirudi kuvichukua.

Tukirudi kwenye sababu tatu za rufaa ni wazi kwamba hati ya talaka haikuwa na sharti lolote la kumtaka Mpinga rufaa kurejesha mahari na baada ya kuwasikiliza mashahidi wa Mkata rufaa pia wameeleza kwamba wao hawakumsikia Mkata rufaa akitoa sharti lolote kwa ajili ya kutoa talaka wala hawakuiona talaka hio ilipokuwa inaandikwa.

Hivyo, Mahkama hii inakubaliana na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa na Kadhi wa Wilaya kwamba talaka tatu zilizotolewa na Mkata rufaa hazikuwa zimefunganishwa na sharti la kurejesha mahari aliyopewa Mpinga rufaa. Hivyo, talaka hiyo imetoka na wala si khuluu. Hivyo, Mpinga rufaa ana haki ya kupewa mahari yake na inaamriwa kwamba

Mkata rufaa ampe Mpinga rufaa vitu vyake vya mahari au apewe thamani ya pesa inayoweza kununua vitu hivyo ndani ya mwezi mmoja.

Hii ni hukumu iliyotolewa na Mahkama hii.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa Jaji

19/1/2023

(Imes.)

Sk. Sameer Zulfikar

Imes.)

Sk. Saleh Hakim

(Imes.)

Sk. Juma Fakih

(Imes.)

Sk. Kani Mkanga

MAHKAMA

Hukumu hii imesomwa leo tarehe 19/1/2023 mbele ya mkata rufaa na wakala wake na bila ya kuwepo mpinga rufaa.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa Jaji

19/1/2023

Nathibitisha kwamba hii ni nakala halisi ya hukumu

……..

MRAJIS

MAHKAMA KUU, ZANZIBAR